

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



TANGAZO KWA UMMA

MABADILIKO YA TARATIBU ZA UDHIBITI UBORA NA UKAGUZI WA MADUHULI

1. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuutaarifu umma kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha muswada wa Sheria (*The Finance Bill 2019*) ambao baada ya kusainiwa utaleta mabadiliko katika Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 (Sura 130) ambapo TBS imeongezewa majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa vyakula na vipodozi, majukumu ambayo yalikuwa yanatekelezwa hapo awali na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA). Utekelezaji wa majukumu haya mapya utanza rasmi tarehe 01 Julai, 2019 kwa kutoa usajili wa majengo ya uzalishaji wa chakula na vipodozi, kusajili na kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa za chakula na vipodozi zinazozalishwa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi.
2. Kufuatia marekebisho hayo ya sheria, TBS inapenda kutoa ufafanuzi kwamba, kuanzia tarehe 01 Julai, 2019:
 - a) Cheti cha usajili wa majengo kilichokwishatolewa na TFDA kwa wazalishaji walioko nchini kitaendelea kutambuliwa na TBS mpaka kwisha kwa muda wake (*Expiry date*) ambao ni miaka mitano. Baada ya muda huo usajili mpya utatolewa kwa utaratibu wa TBS.
 - b) TBS itaendelea na utaratibu wa kutoa usajili wa majengo kwa waombaji wapya kwa kutumia mfumo uliowianishwa, mfumo unaozingatia matakwa ya usalama na ubora kwa pamoja kwa chakula na vipodozi. Aidha, usajili mpya utafanyika kadri vyeti vya usajili wa majengo vilivyopo vitakapokuwa vinaisha muda wake.
 - c) Tofauti na ilivyokuwa awali, upimaji wa sampuli utafanyika mara moja kwa bidhaa zinazokidhi matakwa yote mawili ya usalama na ubora wa chakula na vipodozi kwa mujibu wa viwango husika katika ukaguzi wa mwanzo. Hatua hii inalenga kupunguza gharama na muda wa upimaji hivyo ni vizuri kwa mzalishaji kuhakikisha kwamba anajiandaa vizuri kwa ajili ya kuanza zoezi la udhibiti wa usalama na ubora wa chakula na vipodozi.
 - d) Ikiwa sampuli za ukaguzi wa mwanzo hazitakidhi matakwa ya viwango kuhusu usalama na ubora wa chakula na vipodozi, mzalishaji atashauriwa kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza. Baada ya marekebisho, ukaguzi na upimaji vinaweza kurudiwa kabla ya leseni ya kutumia alama ya ubora kutolewa.

- e) Kufuatia ufaulu kupitia taarifa ya ukaguzi wa kiwanda na taarifa ya vipimo vya maabara, TBS itatoa leseni kuruhusu matumizi ya alama ya ubora kwa bidhaa zinazothibitishwa kwa kutumia viwango vya kitaifa au cheti kwa bidhaa zinazothibitishwa kwa kutumia viwango visivyo vya kitaifa.
- f) Leseni au cheti cha TBS kitakachotolewa kwa utaratibu kama ilivyoielezwa hapo juu katika kifungu e) kitakuwa ni uthibitisho wa usajili wa jengo, usajili wa bidhaa na uthibitisho kwamba bidhaa ni salama na bora kwa vyakula na vipodozi. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za leseni/cheti kwa mwaka na itaondoa mlundikano wa vyeti vya udhibiti kwa mzalishaji.
- g) Kwa upande wa bidhaa za chakula na vipodozi kutoka nje ya nchi, TBS itaendelea kutambua usajili wa bidhaa za chakula na vipodozi kutoka nje ya nchi ambazo zimeshasajiliwa na TFDA, ambapo udhibiti wa bidhaa hizo zinapoingia nchini utafanyika kwa mifumo ya udhibiti ubora iliyowianishwa ili kukidhi matakwa ya usalama na ubora.
- h) TBS itaendelea na utaratibu wa kutoa usajili wa bidhaa za chakula na vipodozi kutoka nje ya nchi kwa waombaji wapya kwa kutumia mfumo uliowianishwa, mfumo unaozingatia matakwa ya usalama na ubora kwa pamoja. Aidha, usajili mpya utafanyika kadri vyeti vya usajili vilivyopo vitakapokuwa vinaisha muda wake.
- i) TBS itaendelea kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa hizo kupitia mifumo iliyopo ya kukagua kabla (*Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards (PVoC) Programme*) au baada ya kufika nchini (*Destination Inspection (DI)*).
- j) Ili kupata cheti cha ubora (*Certificate of Conformity*) chini ya mfumo wa PVoC, mwagizaji wa chakula au vipodozi atawajibika kuambatisha cheti cha usajili wa bidhaa hizo kutoka TFDA (zilizokwisha sajiliwa) au cheti cha usajili cha TBS kwa bidhaa zinazosajiliwa baada ya mabadiliko ya sheria.
- k) Kwa bidhaa ambazo hazijasajiliwa, mwagizaji atawajibika kuwasilisha sampuli TBS kwa ajili ya tathmini na usajili kabla ya kuanza kuagiza rasmi shehena za bidhaa husika. Sampuli itawasilishwa pamoja na fomu ya maombi. Kwa bidhaa zitakazofika nchini bila kusajiliwa, usajili utafanyika sambamba na mifumo iliyowianishwa ya udhibiti ubora na usalama wa bidhaa kutoka nje ya nchi.
- l) Taratibu nyingine zinazohusu mifumo ya udhibiti ubora kwa mujibu wa viwango vya kimataifa yaani ISO/IEC 17067, 17065, 17020 zitaendelea kuzingatiwa kupitia taratibu zilizopo na ambazo hurekebishwa mara kwa mara ili kuleta ufanisi. Taratibu hizo zitahusisha ufuatiliaji wa bidhaa viwandani na sokoni ili kukidhi matakwa ya mifumo na kuhakikisha wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa wanazingatia usalama na ubora wa chakula na vipodozi pamoja na bidhaa nyingine.

3. Ni matumaini ya TBS kuwa wadau na umma kwa ujumla tutazingatia ufafanuzi huu. Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kuwasiliana nasi kupitia anwani zifuatazo:

Mkurugenzi Mkuu
Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
S L P 9524
Dar es Salaam
Simu: +255(022)2450298
Hotline: +080110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS



PUBLIC NOTICE

CHANGE OF PROCEDURES FOR PRODUCT CERTIFICATION AND IMPORTS INSPECTION

1. Tanzania Bureau of Standards (TBS) wishes to inform the general public that the National Assembly of the United Republic of Tanzania has passed the Finance Bill of 2019 which, pending assent by the President of the United Republic of Tanzania, will cause the amendment of Section 130 of the Standards Act No. 2 of 2009, to reflect the additional functions of assuring the quality and safety of food and cosmetics products, which are currently performed by the Tanzania Food and Drugs Authority (TFDA). The implementation of the new functions will commence on 1st July, 2019 and they include registration of production premises for food and cosmetics products and registration and certification of locally produced and imported food and cosmetics products.
2. Following the amendment of the Law, TBS would like to clarify that from 1st July, 2019;
 - a) Premise registration certificates issued by TFDA to local manufacturers will be recognised by TBS till their Expiry Date which is five years. Thereafter, new registration will be issued in accordance with TBS procedure.
 - b) TBS will assume the responsibility for registering premises for new applicants using a harmonized system which observes safety and quality requirements for food and cosmetics products. Moreover, new registrations will be done for expiring premise registration certificates.
 - c) Unlike in the current practice, food and cosmetics samples will be taken and tested once for both quality and safety requirements in accordance with relevant standards for initial inspection. This is aimed at reducing testing costs and turnaround time; thus, manufacturers are advised to make necessary preparations before embarking on food and/or cosmetics products certification processes.
 - d) In case initial inspection samples do not conform to the quality and safety requirements for food and cosmetics, the manufacturer will be advised to make corrective action on observed discrepancies. After taking corrective

action measures, re-inspection and retesting of samples may be conducted before issue of a licence to use the Standards Mark of Quality.

- e) Basing on positive factory inspection and laboratory test results, TBS shall issue a licence to use the Standards Mark of Quality for products certified against national standards or a certificate for products certified against other standards.
- f) A licence or certificate issued by TBS through the procedure specified in e) above shall be attestation of premise registration and product registration and confirmation of safety and quality of food and cosmetic products. This is aimed at reducing annual licencing/certification costs and the piles of licences and/or certificates at the manufacturer's premise.
- g) Concerning imported food and cosmetics products, TBS will recognize the registration of food and cosmetics products issued by TFDA and the certification of those products shall be done through a harmonized system which observes safety and quality requirements for food and cosmetics products.
- h) TBS will assume the responsibility for registering imported food and cosmetics products using a harmonized system which observes safety and quality requirements for food and cosmetics products. Moreover, new registrations will be done for expiring registrations for imported food and cosmetics products.
- i) TBS will proceed with safety and quality assurance of imported products through the existing certification schemes, i.e. Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards (PVoC) Programme or Destination Inspection (DI).
- j) To acquire the Certificate of Conformity under PVoC, the importer of food and/or cosmetics product shall be required to attach the registration certificate issued by TFDA (for registered products) or TBS registration certificate for products registered after the amendment of the Act.
- k) For unregistered products, the importer shall be required to submit samples at TBS for assessment and registration before embarking on importation process. Samples shall be accompanied with a formal request. For unregistered products entering the country, registration shall be done through a harmonized system for registration of imported food and cosmetics products which observes safety and quality requirements for the products.
- l) Other quality and safety assurance measures in accordance with international standards namely ISO/IEC 17067, 17065 and 17020 shall be maintained through existing procedures which are revised from time to time

to enhance their effectiveness. The measures will include market and factory surveillance to ensure conformity to systems requirements and to ensure that manufacturers and distributors of products abide by the safety and quality requirements for food, cosmetics and other products.

3. It is our sincere hope that stakeholders and the public in general will observe this guidance. For more clarifications, do not hesitate to contact us through the following contacts:

Director General
Tanzania Bureau of Standards (TBS)
P O Box 9524
Dar es Salaam
Tel: +255(022)2450298
Hotline: +080110827
Email: info@tbs.go.tz